KARATASI YA TAARIFA

nystateofhealth
The Official Health Plan Marketplace



TAARIFA ZA HARAKA KUHUSU

# Bima ya Meno kwa Familia

**Unastahili huduma ya afya ya bei nafuu.**

**NY State of Health ni bima rasmi ya afya ya New York Marketplace.**

**Jiandikishe leo.**

Mtandaoni katika nystateofhealth.ny.gov

Kwa simu kupitia
1-855-355-5777
TTY
1-800-662-1220

Tembelea In-Person Assistor kwenye info.nystateofhealth.ny.gov/findassistor

NY State of Health inazingatia sheria za haki za raia za Shirikisho zinazotumika na haibagui kwa msingi wa mbari, rangi, asili ya taifa, dini, jinsia, umri, hali ya ndoa/familia, rekodi za kukamatwa, hukumu za uhalifu, utambulisho wa jinsia, mwelekeo wa kingono, sifa za kinasaba, hali ya jeshi, hali ya mhanga wa unyanyasaji wa nyumbani, na/au kulipiza kisasi.

**Huduma ya meno ni sehemu muhimu ya afya na hali yako njema kwa jumla. Lakini kuna mambo ya kuzingatia kabla ya kujiandikisha katika bima ya meno.**

## 1 Je, Qualified Health Plan (QHP) inajumuisha manufaa ya meno kwa familia?

- Ikiwa unahitaji bima ya meno inayofidia watu wazima mbali na watoto, unaweza:
  - Kutafuta QHP nchini mwako zinazojumuisha manufaa ya meno kwa familia kwa kutumia Dental Plan Comparison Tool katika tovuti ya Marketplace kwenye: https://info.nystateofhealth.ny.gov/resource/dental-plan-comparison-tool; au
  - Kufanya ununuzi wa bima ya meno kwa familia ya stand-alone nje ya QHP yako.[1]
- Kwa bima ya meno inayofidia watoto pekee, unaweza kupata manufaa ya meno kwa watoto kupitia QHP yako, au kutoka kwenye bima yako ya meno kwa watoto ya stand-alone.[2]

## 2 Je, bima ya meno kwa familia hufidia nini?

- Mipango ya meno kwa familia ina viwango viwili tofauti vya bima:
  1. Bima ya meno kwa watoto
  2. Bima ya meno kwa watu wazima
- Manufaa ya watoto yana kategoria nne kuu:
  1. Kuzuia/Msingi
  2. Kawaida
  3. Kuu
  4. Othodontia
- Manufaa kwa watu wazima yanaweza kujumuisha baadhi ya kategoria au kategoria zote nne za manufaa.

[1] Lazima uwe umejiandikisha katika Qualified Health Plan (QHP) ili kujiandikisha katika bima ya meno ya stand-alone.
[2] Kwa maelezo zaidi kuhusu manufaa ya meno kwa watoto, tazama *Karatasi ya Taarifa ya NY State of Health Pediatric Dental Coverage*.

nystateofhealth™
The Official Health Plan Marketplace

TAARIFA ZA HARAKA KUHUSU

# Bima ya Meno kwa Familia

## 3 Je, ni huduma gani zinajumuishwa kama manufaa ya meno kwa familia?

| Kategoria ya Huduma | Mfano wa Huduma | Inafidiwa kwa Watoto? | Inafidiwa kwa Watu Wazima? |
| --- | --- | --- | --- |
| Kuzuia/Msingi | Usafishaji, floraidi na vizibaji | Kila wakati | Katika hali nyingi, hutofautiana kulingana na bima |
| Kawaida | Chunguzi, Eksrei, mijazo na utoaji rahisi | Kila wakati | Katika hali nyingine, hutofautiana kulingana na bima |
| Kuu | Upasuaji wa mdomo, meno bandia, vishikizi vya meno na nyama laini za meno | Kila wakati | Katika hali nyingine, hutofautiana kulingana na bima |
| Othodontia | Magango ya kusaidia kulainisha meno | Kila wakati | Katika hali nyingine, hutofautiana kulingana na bima |

- Gharama za kujilipia zinazohusishwa na huduma za meno zinaweza kutofautiana kwa kiwango kikubwa kulingana na bima. Unapaswa kuchagua bima inayojumuisha huduma unazodhani kuwa familia yako inaweza kuhitaji.

## 4 Je, bima ya meno kwa familia itakuwa pesa ngapi?

- Kila bima ya meno ina gharama zisizobadilika. Zinaweza kuwa pamoja na kiasi cha malipo ya bima, makato, gharama za juu zaidi za kujilipia na viwango vya juu zaidi vya manufaa kila mwaka. Gharama hizi zinatofautiana kulingana na bima ya meno.
- Mbali na gharama zisizobadilika, kuna mahitaji ya kushiriki gharama ambazo pia zinatofautiana kulingana na bima. Mahitaji ya kushiriki gharama yanategemea kategoria ya huduma na ikiwa mtoto au mtu mzima anapokea huduma.
    - **Manufaa ya meno kwa watoto** yana kikomo cha juu zaidi cha gharama ya kila mwaka cha kujisimamia cha $350 kwa kila mtoto na $700 na kwa kila familia. Hizi ndizo pesa nyingi *utakazolipa* mwaka wowote wa bima. Hakuna huduma wala vipindi vya kusubiri kwa manufaa ya watoto.
    - **Manufaa ya meno kwa watu wazima** kwa kawaida hayana kikomo cha juu zaidi cha gharama cha kujisimamia. Lakini, huenda kukawa na manufaa ya kila mwaka. Hii ndiyo gharama ya juu zaidi *ambayo bima yako* italipa mwaka mzima wa fidia. Unawajibikia gharama zozote za meno kwa mtu mzima zaidi ya kiwango hiki cha juu. Mbali na hayo, huenda kukawa na vipindi vya kusubiri kwa baadhi ya huduma.[3]

## 5 Je, ninaweza kupata vipi bima ya meno ambayo inanifaa mimi na familia yangu?

- NYSOH Dental Plan Comparison Tool itakuruhusu kulinganisha gharama na manufaa ya bima tofauti za meno kwa watoto.[4] Inaweza kupatikana katika tovuti ya Marketplace kwenye: https://info.nystateofhealth.ny.gov/resource/dental-plan-comparison-tool
- Tovuti ya Marketplace pia ina NYS Provider & Health Plan Look Up Tool, ambayo itakuonyesha orodha ya watoa huduma za meno wanaoshiriki katika kila bima. Inaweza kupatikana kwenye: https://pndslookup.health.ny.gov/

[3] Bima zilizoorodheshwa kwenye zana ya ununuzi ya tovuti ya Marketplace zinabainisha "WP" ikiwa kuna kipindi cha kusubiri kwa huduma zozote zinazofidiwa.
[4] Wakati wa kutafuta bima za meno, hakikisha kuwa unaangalia taarifa ya manufaa ya wanafamilia ambao ni watu wazima na si taarifa za manufaa ya watoto.

Si usted habla un idioma diferente al inglés, los servicios de asistencia de idioma están disponibles gratis para usted. Llame al 1-855-355-5777 (TTY: 1-800-662-1220).
如果您使用的語言不是英語，您可以使用我們的免費語言支援服務。請致電 1-855-355-5777 (TTY: 1-800-662-1220)